Students Name: ………………………………………………………………………

School Name…………………………………………. Index Number ……………

**P320/2**
**FASIHI YA KISWAHILI**
Paper 2
Saa Tatu.
JULAI./AGOSTI

# HES MOCK EXAMINATIONS 2025

## UGANDA ADVANCED CERTIFICATE OF EDUCATION

**FASIHI YA KISWAHILI**
**KARATASI YA PILI**

**(TAMTHILIA)**

**SAA TATU**

**MAAGIZO**

- Karatasi hii ina sehemu nne; A, B, CH na D.
- Mtahiniwa anapaswa kujibu maswali Matatu kwa jumla
- Swali la lazima litoke Sehemu D, na mengine mawili yachaguliwe kutoka Sehemu A, B na CH.
- Mtahiniwa asichague maswali mawili kutoka Sehemu moja.

## SEHEMU A

MABEPARI WA VENISI: WILLIAM SHAKESPEARE

1. Ni kwa namna gani dhamira za mabepari zinasadifu maisha ya wananchi wa leo? (Alama 33)
2. (a) Mapenzi ya masharti yanadhihirikaje katika tamthilia ya Mabepari wa Venisi. (Alama 17)

   (b) Fafanua mafunzo wana jamii wanaiga kutokana na mapenzi haya ya masharti (Alama 16)

**MFALME EDIPODE: SOFOKILE**

3. (a) Kwa kutolea mifano Mwafaka kutoka katika tamthilia, Mfalme Edipode, Fafanua sababu zilizosababisha Anguko la Mfalme Edipode (Alama 17)

   (b) Ni athari gani zilizoikumba jamii ya Thebe baada ya Anguko la Mfalme Edipode (Alama 16)

4. Tamthilia ya 'Mfalme Edipode' ina mengi ya kuwafunza wanajamii. Jadili (Alama 33)

## SEHEMU B

**KIJIBA CHA MOYO: TIMOTHY M AREGE**

5. Jadili Maudhui yanayojitokeza katika tamthilia ya kijiba cha moyo (Alama 33)

6. "Tamthilia ya kijiba cha moyo inaonyesha hali halisi ya vijana humu nchini Uganda" (Alama 33)

**KIMYA KIMYA KIMYA : SAID A MOHAMED**

7. (a) Jadili jinsi mabadiliko yanayojitokeza katika tamthilia ya Kimya Kimya Kimya. (Alama 17)

   (b) Mhusika Mpya ana mengi ya kuwafunza Wanajamii wa leo. Jadili (Alama 16)

8. (a) Tamthilia ya Kimya kimya kimya inaonyesha maadili gani viongozi wa Afrika wakiisoma? Jadili (Alama 16)

   (b) Jadili umuhimu wa muhusika mpya katika ujenzi wa tamthilia ya kimya kimya kimya. (Alama 17)

## SEHEMU CH

9. Soma dondoo hili na kisha ujibu maswali yatakayofuata.

Wamala: Wakati yule mwanamke karani alipoharibu mipango yangu ndipo nilipodhihirikiwa na uhalisia wa shida zetu. Hata hivyo, ninamshukuru kwa kunifanya nitambue kuwa hatutaweza kumudu hali hii tuliyonayo kwa muda mrefu; mimi wewe na watoto.Tunaamka alfajiri mbichi.chai ya mkanda.viazi na maharagwe baridi.mcomomkalewa moshi na uvundo wa mkojo kutoka kitanda cha kake.Tunanawa uso kwa umande kwa kuwa maji ni ghali na hakuna hata tone ndani ya nyumba.kaija anaenda shule.Baridi ya asubuhi inatatarisha meno yake na kuchoma matako yake yaliyo wazi.Kake naye anafukuzana na vipepeo au kuzungukazunguka kimya nje ya nyumba kwa sababu mimi na wewe hatuna lolote la kuzungumza.

Tinka:Tunafaa kumchukuwa huyu msichana kwa daktari bora,wamala.

Wamala:saa nne inatimia.unaanza shughuli zako za ususi au kutayarisha *enguli*.Nina azima gazeti la siku iliyopita na kuanza kupekua kurasa zenye nafsi za kazi.kila ninapo moja inayonifaa,kunakuwepo tena mzigo wa kupata wadhamini watatu ilihali watu wanaonifahamu,ambao ninatangamana nao,na ambao wanaweza kuwa wadhamini ni wale walevi wenzangu;walevi wa republic Bar.wao ndio wanaozijua zaidi shida za nchi zinazoendelea.kisha,inawadia saa ya chakula cha mchana.viazi na maharagwe,mara nyingine kaunga na dodo,na kimya chetu kisichokwisha isipokuwa utani na mara mojamoja ili kuwapa watoto matumaini.jioni ninakwenda republic kukutana na dunia;kukutanana wageni wanaoweza kushawishika na kutununulia pombe.Ninakunywa na kulewa ili nisahau matatizo yangu.Ninarudi nyumbani kwenye maapizo ya kimya kimya na watoto wasiokuwa na tumaini,watoto ambao wanajua mengi lakini hawathubuti kukiri kuwa wanajua.unajikimbiza na kwenda chumbani kulala,name hukufuata ingawa ninajua vyema kuwa sitakiwi nawe wala na chumba chenyewe.Alfajiri nyingine.chai ya mkandaa.viazi na maharage baridi.mchomo mkali wa moshi.siku nenda siku rudi hadi maajilio ya pili ya kisiasa.Hatuwezi tena kuvumilia.

Tinka: Hujaniambia ulipokuwa jana usiku.

Wamala: (kwa kuudhika) usinighasi.

Tinka:ulikuwa wapi?

**MASWALI;**

a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake (Alama 08)
b) Ni mizigo ipi katika dondoo inayokandamiza familia ya wamala? (Alama 12)
c) Jadili udhaifu wa wamala namna unavyojitokeza katika dondoo hili (Alama 06)
d) Ungekuwa Tinka,ungemshauri vipi Wamala? (Alama 06)

e) Taja vitu viwili kutoka dondoo hili vinavyoonyesha kuwa Tinka ni mwanamke mwenye jukumu. (Alama 02)

MKWAMO : MASEREKA LEVI KAHAIKA

10. Soma dondoo hili na kisha ujibu maswali yatakayofuata.

**Kasuku**: Sasa wenzetu wamtusaliti, kidimbwi wameachilia

Bogabuga kote tumekwisha, bali n’tapigana mpaka mwisho

Nasikia amekodi wamanuba, twaumizana. Ya wavaa kasiki tumesahau

Nakumbuka hapo awali, bupomboli kilikuwa

kituo chetu cha biashara. Seko, namuru na

Padilanga vilikuwa vituo vya kubadilishana

mazao na chumvi kutoka katwe

Tulifurahi wasulenge, wadiliko wa budilikilo

nao walishuhudia muamala kamili sote kujuliana, sasa twaumana kipanzi

Lakini subiri, mtego wa panya, ni kwa waliomo na wasiomo

Nami wa mukidi babu, kutamauka nimeshakufa ni ahadi nimeishatoa kwa hivyo ewe jemadari uliye bora fanya hima kimbia kilimani kawambie wapiganaji huko…, wasilale kamwe, uanawake wetu wamejiunga

Kasikinya hapa amepatuliza, ni shujaa name sina wasi.

Haya enenda Yarwa mpole.

**Kasikinya**: Jana usiku kucha tumelinda kule chini kidimbwini walioko nao hawakutambua.

Ningewavamia lakini walikuwa wengi; wengi kiasi cha kutumeza wazima, bali kwa hila

nikawapotosha kutafuta njia kuelekea marujubu nikawelekeza sehebu mbali

na hapa pa Waruzi.

Nyuma wakageuka kudhani wamepotea. Kwa sasa wanawake wetu shujaa waende punde

huko kidimbwini, wajifanye wema na waaminifu, nao watujulishe nia za vibaraka, niliona

maji ya kunde bunduki mkononi kapakata.

Roho ikanidundadunda lakini nikajizatiti nisijemwaga mtama wangalipo kuku. Nina uhakika

wanakusudia hapa…, lakini iliyo bora akili, tuwe tayari wakati wowote.

Tusiwavamie tujihami hapa tulipo tusubiri hadi waingie sehemu petu wasikojua tuliko kasha tuwateketeze na kuikomboa karuhoko.

***(Yarwa anaondoka. Wasichana wapiganaji wawili wanaingia)***

**Wasichana:** Mfalme unayewashinda wote, kasuku wa Bupomboli Hatutakuacha pekee,

katika vita hivi vya mtu mweusi.

Nasi jana tulimshuhudia maji ya kunde. Watu wetu wengi wamemfuata lakini usife moyo.

Vijana kwa wazee wameapa kutokubali. Ziwa letu zuri Mwitanzige hatutamwachia maji

ya kunde aparamie na vibaraka.

Mabikira wapole wanakasuku, mabinti wasifikao, kazi umetuelekeza, twaomba uende

ukatulie kijumbani mwako nasi kwa ulinzi wako tu tayari.

Nyuta na mishale tayari, ng'ao tumebeba yote ni kwa ulinzi wako, tumaini letu ndiwe

ukifa nasi twajua watumwa, ya utumwa tumesikia hatutaki kushuhudia; huko kwingine

wakakubali wanao kuuza kwa silaha. Kwetu we ni ngao, kutukinga ukafurahia, hii ni

zamu yetu tukukinge ewe mfalme

**MASWALI**

a) Liweke dondoo hili katika mkutadha wake. (Alama 08)

b) Ukitoa mifano kutoka dondoo,fafanua mambo muhimu tano yanayozingatiwa na mwandishi katika dondoo. (Alama 10)

c) Ni jambo gani lililosababisha dondoo hii? (Alama 04)

d) Jadili uhusiano uliopo baina ya mhusika Kasuku na Kasikinya katika dondoo. (Alama 04)

e) Mwandishi anakusudia nini katika dondoo hili? (Alama 04)

f) Kulingana na yaliomo,mwandishi anamaanisha nini akisema;

i. Mtego wa panya ni kwa waliomo na wasiomo. (Alama 02)

ii. Roho ikanidunda lakini nikajizatiti nisijemwaga mtama wangalipo kuku

## SEHEMU D

## KILIO CHA HAKI: ALAMINI MAZRUI

11. Dhuluma ni mandhui pekee yanayojitokeza katika mchezo, "Kilio cha haki" Jadili (Alama 33)

*12.* (a) Jadili mafunzo unayopatapata kulingana na matukio yaliyomo katika tamthilia ya Kilio Cha Haki. (Alama 20)

(b) Jadili suala la Uzalendo katika mchezo huu wa Kilio Cha Haki (Alama 13)

## CHEMA CHAJIUZA: INNOCENT AGUME

13. Eleza wasifu wa wahusika wafuatao katika Tamthilia ya Chema Chajiuza

i) Kunihira

ii) Kwatampola

iii) Nabaganzi (Alama 33)

14. Wafanyakazi na waajiri wao hupata maadili yepi baada ya kusoma Tamthilia ya Chema Chajiuza? Eleza (Alama 33)

***MWISHO***